TANGAZO LA SERIKALI Na. 725 la tarehe. 16/8/2024

SHERIA YA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI,
(SURA YA 297)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 109)*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA MAZINGIRA YA KAZI ZA MWAKA 2024

Jina

TS. Na. 289 la 2023

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Mazingira ya Kazi za mwaka 2024 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Mazingira ya Kazi, ambazo katika Kanuni hizi zimerejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 2

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 2 kwa kufuta kifupisho "(dBA)" kilicho kwenye tafsiri ya maneno "kipimo cha sauti" na badala yake kuweka kifupisho "dB(A)".

Marekebisho ya kanuni ya 4

3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 4-

(a) kwa kufuta na kuandika upya kanuni ndogo ya (1) kama ifuatavyo:

"(1) Mwajiri hatamruhusu mfanyakazi kufanya kazi katika mazingira ambayo wastani wa halijoto ya balbu kavu iliyopimwa kwa kipindi cha muda wa masaa manne ni chini ya nyuzi joto ya sentigredi 6.

(b) kwa kongeza mara baada ya kanuni ndogo ya kwanza kanuni ifuatayo:

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), mwajiri atachukua hatua zinazofaa kumlinda mfanyakazi dhidi ya baridi na kuchukua tahadhari zote muhimu kwa usalama wa mfanyakazi huyo,

Isipokuwa pale ambapo kazi ya nje

inafanywa, mwajiri atachukua hatua hizo na tahadhari kama hizo katika mazingira ambayo halijoto ya balbu kavu ni chini ya nyuzi joto ya sentigredi 6 wakati wote.”;

(c) kwenye maneno ya ufunguzi katika kanuni ndogo ya (2) kwa kufuta maneno “nyuzi joto 0” na badala yake kuweka maneno “nyuzi joto ya sentigredi 0”; na

(d) kwa kurekebisha mpangilio wa kanuni ndogo ya (2) mpaka (5) na kuwa kanuni ndogo ya (3) mpaka (6) mtawalia.

Dodoma
……………., 2024

RIDHIWANI J. KIKWETE,
*Waziri wa Nchi,*
*Ofisi ya Waziri Mkuu,*
*(Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)*